TANGAZO LA SERIKALI NA. 928 la tarehe 15/11/2024

SHERIA YA VIWANGO,
(SURA YA 130)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 21B(2)(a))*

KANUNI ZA UONGEZAJI WA VIRUTUBISHI KWENYE CHAKULA ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Jina* *Kanuni*


SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UONGEZAJI WA VIRUTUBISHI KWENYE CHAKULA

4. Uongezaji wa lazima wa virutubishi kwenye chakula.
5. Uongezaji wa hiari wa virutubishi kwenye chakula.
6. Uhakiki wa Usalama na Ubora.
7. Zuio la kuzalisha, kuingiza nchini na kuuza chakula kisichoongezwa virutubishi.
8. Kukidhi matakwa ya kifungashio cha chakula kilichoongezwa virutubishi.
9. Idhini ya kuingiza nchini, kuzalisha au kusambaza chakula kisichoongezwa virutubishi.
10. Matumizi ya nembo ya uongezaji wa virutubishi kwenye chakula.
11. Masharti ya ufungashaji, uwekaji lebo na uhifadhi wa chakula kilichoongezwa virutubishi.
12. Ukaguzi, kushikilia na uchunguzi wa chakula.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA

13. Makosa na adhabu.

MAJEDWALI

SHERIA YA VIWANGO,
(SURA YA 130)

---

KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 21B(2)(a))*

KANUNI ZA UONGEZAJI WA VIRUTUBISHI KWENYE CHAKULA ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uongezaji wa Virutubishi kwenye Chakula za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwenye chakula kilichofungashwa, ambacho kinatakiwa kuongezwa virutubishi kwa ajili ya matumizi ya binadamu ikiwa kimeingizwa au kuzalishwa nchini.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"chakula" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"chakula kibebaji" maana yake ni unga wa ngano, unga wa mahindi, mafuta ya kula yaliyosafishwa, na chumvi kinachotumika kama kibebaji cha virutubishi wakati wa uongezaji virutubishi kwenye chakula;

"chakula kilichoongezwa virutubishi" maana yake ni chakula ambacho kimeongezwa virutubishi kwa mujibu wa kanuni hizi;

"chakula kilichofungashwa" maana yake ni chakula kilichosindikwa ili kuongeza muda wake wa matumizi, kikiwa kimefungashwa, kimewekewa lebo na kimekidhi viwango vilivyoainishwa na kipo tayari kwa ajili ya matumizi kwa mlaji, na inajumuisha chakula nyongeza;

"chumvi" maana yake ni chumvi inayoliwa ambayo ni

chembe chembe ngumu, yenye rangi, nyeupe, au nyeupe iliyofifia, au kijivu isiyokolea na yenye kiwango kikubwa cha madini ya sodiamu kloridi yanayopatikana baharini, miamba ya ardhini, miamba ya chumvi, au nyongo ya chumvi na ambayo haijachafuliwa na vumbi, uchafu, udongo wa mfinyazi, changarawe, mchanga au aina nyingine yoyote ya takataka au uchafu;

"eneo" lina maana sawa kama lilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"fotifikanti" maana yake ni mchanganyiko maalum ulioainishwa wenye virutubishi vinavyokusudiwa kuongezwa kwenye chakula;

"kifungashio" lina maana sawa kama lilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"kirutubishi" maana yake ni vitamini ya asili au iliyotengenezwa, madini, au elementi ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa kawaida, maendeleo na uimarishaji wa afya;

"mafuta ya kula" maana yake ni mafuta ya kula yanayotokana na mimea au wanyama kwa ajili ya kuuza kwa matumizi ya binadamu;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya Sheria;

"mzalishaji" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"onesha" maana yake ni kuonesha chakula kilichoongezwa virutubishi kwa ajili ya kuuzwa;

"primiksi" maana yake ni mchanganyiko wa fotifikanti na vizimuzi maalum unaotumika kuongeza virutubishi kwenye chakula;

Sura ya 130 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Viwango;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Viwango Tanzania lililoanzishwa chini ya Sheria;

"uongezaji wa virutubishi kwenye chakula" maana yake ni uongezaji wa virutubishi kwenye chakula kwa lengo la kuzuia au kudhibiti upungufu wa virutubishi katika jamii au kundi maalum katika jamii;

"kuuza" inajumuisha kitendo cha kubadilishana bidhaa

bila kuhusisha fedha, kuweka hadharani, kutangaza nia ya kuuza na kuuza nje ya nchi au kwa madhumuni ya kuuza, na umiliki kwa madhumuni yoyote ya kuuza, kuuza nje ya nchi, biashara au kuzalisha; na

"Viwango vya Kitaifa" maana yake ni viwango vya kitaifa vilivyoidhinishwa na Waziri chini ya Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## UONGEZAJI WA VIRUTUBISHI KWENYE CHAKULA

Uongezaji wa lazima wa virutubishi kwenye chakula

4.-(1) Uongezaji wa virutubishi kwenye chakula kilichofungashwa utakuwa ni lazima kwa vyakula vifuatavyo:

(a) unga wa ngano;
(b) unga wa mahindi;
(c) mafuta ya kula yaliyosafishwa; na
(d) chumvi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), uongezaji virutubishi wa lazima utahusisha virutubishi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

TS. Na. 683 la 2021 681 la 2021

(3) Uongezaji virutubishi kwenye chakula utakuwa ni sehemu ya mchakato wa uthibitishaji na usajili wa bidhaa kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Majengo na Uthibitishaji wa Bidhaa na Kanuni za Usajili wa Bidhaa zinazoingizwa Nchini na Uthibitishaji wa Bechi.

(4) Katika uzalishaji wa chakula kilichoongezwa virutubishi, mzalishaji atatumia fotifikanti au primiksi ambazo zinakidhi viwango vya kitaifa au viwango vingine vyovyote vinavyotambuliwa na Shirika.

Uongezaji wa hiari wa virutubishi kwenye chakula

5. Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, mzalishaji mwenye nia ya kuongeza virutubishi kwenye chakula kingine chochote ambacho siyo sehemu ya chakula kibebaji cha lazima kinachodhibitiwa chini ya Kanuni hizi, atazingatia viwango husika vya kitaifa.

Uhakiki wa Usalama na

6.-(1) Mzalishaji wa chakula kilichoongezwa virutubishi-

Ubora

(a) ataandaa, kudumisha na kufuata taratibu za uhakiki wa usalama na ubora wakati wote wa uzalishaji; na

(b) atahakikisha bidhaa inayozalishwa inakidhi masharti ya Kanuni hizi na kanuni zingine zozote zilizotengenezwa chini ya Sheria.

(2) Mtu anayeuza, kusambaza, kuhifadhi, kuonesha, kuagiza toka nje ya nchi au kuweka hadharani kwa lengo la kuuza chakula chochote atazingatia vigezo vya usalama na ubora.

Zuio la kuzalisha, kuingiza nchini na kuuza chakula kisichoongezwa virutubishi

7. Mtu hataruhusiwa kuzalisha kwa ajili ya kuuza, kusambaza, kuhifadhi, kuonesha, kuingiza nchini au kuweka wazi kwa ajili ya kuuza chakula chochote kinachodhibitiwa chini ya Kanuni hizi isipokuwa chakula hicho kinakidhi Viwango vya Kitaifa vya chakula kilichoongezwa virutubishi.

Kukidhi matakwa ya kifungashio cha chakula kilichoongezwa virutubishi

8.-(1) Mtu anayehifadhi, kuonesha, kuuza au kusambaza chakula kilichoongezwa virutubishi atahakikisha kifungashio kilichotumika kinakidhi masharti ya Kanuni hizi.

(2) Mtu hataruhusiwa kuuza au kusambaza chakula kilichoongezwa virutubishi katika kifungashio-

(a) kilichoharibika; au

(b) ambacho taarifa zake hazisomeki au zimebadilishwa kinyume cha Sheria.

Idhini ya kuingiza nchini, kuzalisha au kusambaza chakula kisichoongezwa virutubishi

9. Shirika baada ya kujiridhisha kuwa kuna dharura au upungufu wa chakula linaweza, kuidhinisha uingizaji nchini, uzalishaji au usambazaji wa chakula kisichoongezwa virutubishi, baada ya kupokea fomu ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Matumizi ya nembo ya uongezaji wa virutubishi kwenye chakula

10.-(1) Mtu anayezalisha au kuingiza nchini chakula kilichofungashwa chini ya Kanuni hizi baada ya kupata leseni au kusajiliwa na Shirika atatumia nembo ya uongezaji wa virutubishi kwenye chakula kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Mtu ambaye-

(a) kwa hiari ataongeza virutubishi kwenye chakula ambacho hakija ainishwa kwenye kanuni ya 4; au

(b) atazalisha au kuingiza nchini chakula kisichoongezwa virutubishi kwa mujibu wa kanuni ya 9,

hataruhusiwa kutumia nembo ya uongezaji virutubishi kwenye chakula.

Masharti ya ufungashaji, uwekaji lebo na uhifadhi wa chakula kilichoongezwa virutubishi

11. Mtu hataruhusiwa kufungasha, kusababisha kufungasha au kuhifadhi chakula kilichoongezwa virutubishi, isipokuwa ufungashaji au uhifadhi umefanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kitaifa au viwango vingine vyovyote vinavyotambuliwa na Shirika.

Ukaguzi, kushikilia, na uchunguzi wa chakula
TS. Na. 682 la 2021

12.-(1) Mkaguzi wakati wowote au pale ambapo kuna ukiukwaji wa Kanuni hizi anaweza, kukagua eneo lolote ambalo chakula kinazalishwa, kinauzwa, kinasambazwa, kinaoneshwa, kimefungashwa au kimehifadhiwa na kuchukua hatua stahiki ikijumuisha kushikilia bidhaa zisizokidhi viwango kwa mujibu wa Kanuni za Kuondoa, Kushikilia na Kuteketeza Bidhaa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Mkaguzi anaweza kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa maabara au uchunguzi mwingine wa chakula kilichoongezwa virutubishi kwa lengo la kuhakikisha kama chakula kinakidhi vigezo vya usalama na ubora.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkaguzi anaweza kuchunguza au kukagua nyaraka zozote zinazohusika kwa lengo la kuhakikisha uhalali wa nyaraka hizo.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Makosa na adhabu

13. Mtu anayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni mia moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua

miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

VIRUTUBISHI VYA LAZIMA VYA KUONGEZA KWENYE CHAKULA

| Chakula kibebaji | Kirutubishi | Fotifikanti |
|---|---|---|
| Unga wa ngano | Madini chuma | Sodiamu Madini Chuma Asidi ya EDT<br>Ferasi Fumarate |
| | Zinki | Zinki Oksaidi |
| | Vitamini B12 | Vitamini B12 |
| | Foleti | Asidi ya Foliki |
| Unga wa mahindi | Madini chuma | Sodiamu Madini Chuma Asidi ya EDT<br>Ferasi Fumarate |
| | Zinki | Zinki Oksaidi |
| | Vitamini B12 | Vitamini B12 |
| | Foleti | Asidi ya Foliki |
| Mafuta ya kula yaliyosafishwa | Vitamini A | Retinili Palimiteti |
| Chumvi | Madini joto | Potasiamu Ayodeti |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9)*

MAOMBI YA KIBALI CHA KUINGIZA NCHINI, KUZALISHA AU KUSAMBAZA CHAKULA KISICHOONGEZWA VIRUTUBISHI

(Fomu tofauti ijazwe kwa kila bidhaa)

1. Taarifa za muombaji

| |
|---|
| Jina la muombaji: …………………………………………… |
| Anuani ya posta: ………………………………………………….<br>…………………………………………………………………………………….. |
| Anuani ya makazi: ……………………………………………<br>…………………………………………………………………………………… |
| Namba ya simu: …………………………….………………... |
| Barua pepe: …………………………………………… |
| Tovuti: ………………………………………… |

*Tangazo la Serikali na. 928 (Linaendelea)*

Namba ya leseni ya biashara ya muombaji ……………………………………….
Namba ya usajili wa kampuni…………………………………….

2. Taarifa za bidhaa

(a) Jina la bidhaa: ……………………….……………………….
(b) Taarifa za mzalishaji:………………… ……….
Anuani ya posta: ……………………………………………….
Anuani ya makazi: ………………………………………………………………..
Namba ya simu: ……………………………..
Barua pepe: ………………..
Nchi inakotoka: ………………………………….

Kiasi: ……………… kilogram/metriki tani/lita za ujazo…………………………..

3. *Sababu* ya maombi ya kibali cha kuingiza nchini, kuzalisha au kusambaza chakula kisichoongezwa virutubishi *(Weka vema panapohusika)*

[ ] Kusaidia mahitaji ya chakula wakati wa hali ya dharura kama ilivyoidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya uhakika wa chakula.
[ ] Upungufu wa mahitaji ya fotifikanti zinazohitajika katika uongezaji wa virutubishi kwenye chakula kama ilivyoidhinishwa na Taasisi ya Umma yenye dhamana ya kusimamia lishe.
[ ] Sababu nyingine (ainisha): ……………………………………………………………….

4. Tamko la muombaji

Mimi, …………………………………………………………………………ninatamka kwamba, taarifa zilizomo kwenye fomu hii ya maombi ni za kweli na sahihi.
Saini:………………………Tarehe:……………………………………..
Cheo:…………………………………
Muhuri wa ofisi:……………………………….

5. KWA MATUMIZI YA OFISI TU
Kibali kimetolewa/kimekataliwa cha kuingiza nchini/kuzalisha/kusambaza chakula kisichoongezwa virutubishi *(Futa maneno yasiyohusika)*

Jina la bidhaa na muda wa kibali: …………………………………………………

Sababu za kukubali au kukataa kuingiza nchini/kuzalisha/kusambaza chakula kisichoongezwavirutubishi……………………………………………………………
Namba ya Kibali: …………………… Kilichotolewa (tarehe) ………..………….
Kimeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu
Jina:……………………………………………..
Saini: ……………………………………………
Muhuri wa ofisi:…………………………………

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10 (1))*

NEMBO YA UONGEZAJI WA VIRUTUBISHI KWENYE CHAKULA

Dodoma,
22 Oktoba, 2024

SELEMANI SAIDI JAFO
*Waziri wa Viwanda na Biashara*